# KENYA NATIONAL EXAMINATION COUNCIL
# REVISION MOCK EXAMS 2016
## TOP NATIONAL SCHOOLS

**BAHATI GIRLS HIGH SCHOOL**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA 2**
**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**

**SCHOOLS NET KENYA**
Osiligi House, Opposite KCB, Ground Floor
Off Magadi Road, Ongata Rongai | Tel: 0711 88 22 27
E-mail:infosnkenya@gmail.com | Website: www.schoolsnetkenya.com

## BAHATI GIRLS HIGH SCHOOL KCSE TRIAL AND PRACTICE EXAM 2016

**102/2**

**Karatasi ya 2**

**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**

**1. UFAHAMU**

(a) Kuingiza bidhaa au gesi zisizohitajika katika mazingira.

(b) Huongeza gesi zinazoharibu ukanda wa ozoni.

(c) Gesi zinazotokana na jokofu, marashi ya upakiaji bidhaa huharibu ukanda wa oksijeni unaokinga miale mibaya ya jua.

(d)

-Mvua ya asidi huua mimea, kuathiri majengo na kuwaua wanyama.
-Madini ya risasi huathiri mfumo wa akili ya binadamu.
-Huweza kusababisha majanga ya moto.
-Huathiri afya za binadamu.

(e) Idadi kubwa ya magari – magari haya hutoa moshi unaochanganya gesi ambazo huungana na nyingine zinazoletwa na viwanda vikubwa.

(f)

-Uchafuzi wa hali ya anga.
-Uchafuzi wa kiajali.

(g)

-Msambao – maenezi.
-Makopo – vyupa vya plastiki. Aondolewe hadi alama 6.
-Sarufi – alama 3
-Hijai –alama 3
-Jumla –alama 6

**2. UFUPISHO**

(a) - Ukeketaji ni upasuaji unaofanyiwa wasichana na wanawake.

- Hupatikana barani Afrika na sehemu nyingi ulimwenguni.
- Umri ambapo ukekeaji hufanyika hutegemea jamii.
- Mwanamke anaweza kufanyiwa ukeketaji siku chache baada ya kuzaliwa au baada ya kujifungua mtoto wake wa kwanza.

- Jamii huthamini amali hii kwani ni hatua ya mpito wa maisha.
- Hufungamana kuwapa wasichana mafunzo kuhusu kanuni za uzazi, malezi na ndoa.
- Dhimu kuu ni kuwapunguzia wanawake uchu na kuhifadhi ubikira.
- Wanaume husisitiza tohara kama kigezo cha mwanamke kuolewa.
- Wanawake wenyewe huhakikisha watoto au wajukuu wanapashwa tohara.

(b)
-Ukeketaji una madhara na unadhalilisha wanawake.
-Wanawake huvuja damu na aghalabu huaga dunia.
-Wale wanaopona huwa na hatari ya kuambukizwa maradhi ya zinaa.
- Madaktari wanadai uchungu wa uzazi huwa mwingi na hudumu muda mrefu.
- Wembe utumiwao hauchemshwi kuua viini.
-Wasichana wanaotahiriwa nguvu za kinga dhidi ya magonjwa hupungua.
- Ukeketaji humdhalilisha mwanamke na unastahili kulaaniwa. (Aondolewe hadi alama 3)

**3. MATUMIZI YA LUGHA**

d) (i) Rehema alikimbia kuja upande nilipokuwa / upande wangu kunilaki / kwa niaba. (alama 1)
(ii) Rehema alinitoroka kwenda mbali nami. (alama 1)
e) Ukisamehewa na Mola utapata amani mchana kutwa. (alama 2)

d) Kiambishi 'ku'
- Hutumiwa kama kiambishi ngeli cha nomino zinazoundwa kutokana na vitenzi (kuchuuza).
-Hutumiwa kama kiambishi cha upatanisho wa kisarufi (mf. K<u>u</u>igiza k<u>u</u>zuri k<u>u</u>lituzwa)
-Hutumiwa kama kiambishi cha kuonyesha mahali lakini bila kudhihirisha sehemu mahususi (mf. huku)
-Kiambishi hutumiwa pamoja na vitenzi vyenye silabi moja (mf. ku-cha, ku-fa).
-Hutumiwa kusimamia wakati katika ukanusho wa sentensi za wakati uliopita (mf. hakuenda).(Hoja zozote 2 x 1 = alama 2)

(b) (i) Ngoma zile zinalia vibaya kwa kuwa zimepasuka. (alama 1)
(ii) Ni milango ipi iliyofungwa na ninyi tulipoenda? (alama 1)

(c) (i) Ahaa! – Hutumiwa kuonyeshea furaha au hata mshangao; huonyesha pia mgutuko baada ya kutambua jambo mf. Ahaa! Alisema na kuruka juu kwa furaha baada ya kusikia kuwa alifuzu kazi.

a. Taib! Hutumiwa kuonyesha kupendezwa na jambo au kukubaliana na hali fulani. Mf. Taib! Naona umefaulu sasa.

(d) Walimu wana <u>wajibu</u> wa kufanya wanafunzi wao wakomae vyema. (alama 2)

(e) (i) Fauka ya kuwa na haki za watoto, watoto wanakumbana na dhiki kubwa. (alama 1)

(ii) Licha ya tarishi kula staftahi, alienda ofisini. (alama 1

(f) (i) Heshima – staha, taadhima. (alama 1)
(ii) Ruhusa – kibali, idhini. (alama 1)

(g) <u>Maana</u>
(i) Enda jongomeo – Fariki, kufa (alama 1)
(ii) Piga unyende – Lia kilio kinachoonyesha hofu. (alama 1)

(h) (i) Neno "kile" kama kivumishi.
K.m kiti <u>kile</u> kinafanana na cha kakangu (baada ya jina).
(ii) 'Kile' kama kiwakilishi.
Mf. Kile kilinunuliwa juzi kwa bei ghali (badala ya jina)

(i) Anguka chubwi – Kuanguka majini au kwenye kitu kiowevu.
Anguka tapwi – Kuanguka matopeni.

(j) Atunge sentensi kuonyesha:
(i) Gati – Ni mahali pa kushika pwani kutoka chomboni.
(ii) Kati – Ni baina ya kitu na kingine.
*Waandike sentensi za kutofautisha maana kwenye kila jozi. Mtahiniwa akitoa maana bila sentensi, atuzwe nusu ( ½) alama badala ya alama moja.*

(k) (i) Yenye
(ii) Kwenyewe (alama 2)

(l) (i) La – lisha
(ii) nywa – nywisha / nywesha
(iii) fa – fisha (alama 3)

(m) Ng'ombe
Nyanya

Ngano (Mwalimu akadirie mengine) (alama 3)

(n) Samaki huogelea mtoni. (alama 3)
S ⟶ KN(N) + KT(T + E)

(o) Ukimwona mwambie namwita.

(p) Alim-awali.
ea-tamati

(q) (i) Amri
(ii) Kitenzi kishirikishi kipungufu.

(r)

- Kwa niaba

- Kumpa ujumbe kupitia kwa simu.
*Makosa ya sarufi yaondolewe kila yanapotokea hadi nusu ya alama alizotuzwa katika kila kijisehemu. Makosa ya hijai yaondolewe hadi alama 3.*

**2. ISIMU JAMII**

(a)

- Huunganisha watu wa taifa.
- Huziba mipaka ya kikabila.
- Hukuza utamaduni wa kiafrika.
- Hukuza uzalendo.
- Hutambulisha watu wa taifa fulani.
- Huleta maendeleo ya kijamii, kisiasa, kiuchumi na kisayansi kutokana na umoja wa kitaifa kilugha.
- Hufanikisha harakati za uongozi.
- Husawazisha watu kilugha kwa sababu hisia zitakuwa sawa. (Hoja zozote 3x1 = alama 3)

(b) (i) Lugha ya mwanasiasa.

a. Husema mengi ingawa huwaambia watu kuwa ana machache.

b. Hujisifu mwenyewe.

(c)
(i) Watu hawazingatii usanifu wa lugha tena na hutumia sheng' pakubwa katika mazungumzo yao.

(ii) Watumiaji wa sheng' hawazingatii umri na vyeo vya wanaozungumziwa.
(iii) Tatizo la sheng' limekuwa chanzo cha kuzorota kwa viwango vya lugha katika shule.

(Hoja 3x1 = alama 3)

**MAKOSA YA HIJAI**

Haya ni makosa ya maendelezo na yanatatiza matamshi.

1) Kutenganisha neno kama aliye kuwa.

2) Kuungaisha maneno kama kwavile

3) Kukata silabi vibaya kama ng-ano.

4) Kuandika herufi isiyofaa katika neno kama tata badala ya dada.

5) Kuacha herufi inayofaa katika neno kama tbia.

6) Kuongeza herufi isiyofaa katika neno kama 'piya'

7) Kuacha alama inayotarajiwa kuwepo katika neno kama 'ngombe' badala ya ng'ombe.

8) Kutoandika kistari cha kukata neno ufikiapo pambizo au mwisho wa mstari.

9) Kuandika neno kwa ufupi k.v.

- Kila kosa liadhibiwe mara mbili kwenye maneno mawili tofauti.

**MAKOSA YA SARUFI**

Haya ni makosa yanayotatiza maana au kukiuka sheria za sarufi.

1) Kuakifisha vibaya k.m. nukta, koma n.k.

2) Kutumia herufi kubwa au ndogo visivyo / pahali si pake.

3) Matumizi mabaya ya ngeli, viambishi, nyakati, mnyambuliko n.k.

4) Kuacha au kuongeza neno katika sentensi.

5) Kuchora kistari mwanzo wa sentensi.

6) Miundo mibaya ya sentensi.

**MATUMIZI YA HERUFI KUBWA**

1) Mwanzo wa sentensi

2) Majina ya pekee kama:

(i) Watu

(ii) Mahali k.m. miji, nchi n.k.

(iii) Siku za juma k.m. Ijumaa

(iv) Majina ya miezi k.m. Januari

(v) Mashirika na taasisi.

(vi) Masomo k.m. Fizikia.

(vii) Vitabu kama Asali Chungu.

(viii) Makabila k.m. Hausa.

(ix) Lugha k.m. Kiswahili.

(x) Majina ya Mungu kama Rabuka, Yahweh n.k.

- Tuza alama zaidi kabla ya kuadhibu kosa la hijai.
  Usiondoe zaidi ya nusu ya alama ulizotuza katika jibu la mtahiniwa